HiNation® HiLight™

Kifaa bibebwacho kinachotumia nishati ya jua
MWONGOZO WA MTUMIAJI

Kitoa cha USB cha kuchaji vifaa vya kielek-troniki.

Ingizo ndogo la USB la kuchaji betri la HiLight kutoka kwa gridi au USB.

Kifuniko cha taa kinachokunjika kilichotengenez-wa na mpira wa kujikinga

Seli za nishati ya jua

VIPENGELE



Kitufe cha HiLight

Kionyesha kiwango cha kuchaji na betri



Kionyesha onyo

Ukanda wa kitambaa wa kunyumbulika

Taa ya LED

HiNation® HiLight™ Utatuzi wa seli ya nishati ya jua ya mkono isiyonyooka unatoa:
• Mwangaza angavu na ulio salama, na
• Chaja ya simu rununu ikiwa ni pamoja na Blackberry na iPhone, iPad, kamera dijiti, GPS, MP3, nk.



Mwangaza wa jua kwa masaa 10 | Mwangaza kwa masaa 10-20 | AU | <Kuchaji simu 10 za rununu

WASILIANA
Barua pepe info@hination.com
Simu +46(0)707-949280

www.hination.com – Watumizi wa nje
www.hination.org – *Masoko yanayoibuka*



KUANZA
Kuchaji kifaa chako kutoka kwa HiLight
- Unganisha kifaa chako kwa HiLight kwa kutu mia kebo ya USB.
- Bonyeza na ushikilie kitufe cha HiLight kwa sek. 1 ili uanzishe kuchaji (LED za kijani zinawaka).
- LED za kijani thabiti: HiLight inachaji kifaa chako.
- Tenganisha kifaa chako wakati kimejaa chaji au wakati betri la HiLight liko tupu (LED za kijani zinazima) ili ulinde betri.
- Unaweza kuchaji kifaa chako wakati HiLight inaendelea kuchaji kwa jua.

Kutumia taa, bonyeza kitufe cha HiLight:
Kwa mwangaza wa kawaida, mpaka masaa 20 - bonyeza mara moja. Kwa mwangaza mkali, mpaka masaa 10 - bonyeza tena, Kuzima taa - bonyeza mara ya tatu.
Ausschalten der Lampe – Drücken sie ein drittes mal.



Unapotumia taa, itapepesa mara 3 kuonyesha kwamba betri la HiLight liko karibu kuisha.

Kuchaji HiLight kwa jua:
Weka HiLight kwenye jua na elekeza seli za nishati ya jua upande wa jua. LED za kijani zinazopepesa zinaonyesha inachaji. Kumbuka: Vivuli au mawingu yanapunguza ufanisi wa kuchaji.



Kuchaji HiLight kupitia USB Ndogo:
Unganisha HiLight kwa gridi au USB ya kompy-uta ukitumia kebo ya USB Ndogo. LED za kijani zinazopepesa zinaonyesha inachaji. Kebo haijaju-muishwa.

MODI YA BUMBWAA
Tumia modi ya bumbwaa kudumisha viwango vya betri na uweke HiLight ikiwa tayari kutumiwa baada ya hifadhi ya muda mrefu.
Kuingia kwa modi ya bumbwaa, bonyeza na us-hikilie kitufe cha HiLight kwa sekunde 10, kutoka kwa modi ya bumbwaa, bonyeza kitufe cha HiLight mara moja.

VIONYESHA HILIGHT

Kionyesha kuchaji:
Bonyeza na ushikilie kitufe cha HiLight kwa sekunde 1 ili oune kiwango cha betri ya HiLight, kinachoony-eshwa na LED za kijani:
0 = tupu
1 = karibu kuisha (chini ya 30%)
2 = chini ya nusu (30-60%)
3 = zaidi ya nusu (60-90%)
4 = imejaa (90-100%)

Kitufe cha HiLight

Warnanzeigen:
LED nyekundu ambayo inaonyesha kuchaji/kutoa chaji imesimama kiotomatiki kwa sababu:
- Betri la HiLight liko nje ya kiwango cha hali ya joto cha utendaji, au
- HiLight imepakiwa kupita kiasi kwa kuchaji vifaa vingi zaidi.

Kuseti upya, bonyeza kitufe cha HiLight kwa sekunde 1.

UTENDAJI
(kunalingana na aina ya simu rununu, mahali nk.)
masaa 10 ya mwangaza safi wa jua hutoa betri lililojaa chaji kamili, ambalo linatoa
- Masaa 20 ya mwangaza (kwa kiwango cha kawaida), au
- <kuchaji simu 10 za rununu, au
- Masaa 14 ya utumiaji wa GPS

CHUNGA
- Hakikisha umefunga kifuniko cha USB wakati wowote hauchaji.
- Unapochaji betri la HiLight kupitia USB Ndogo, tenganisha kebo wakati betri la HiLight limechaji kabisa.
- Kama kifuniko cha USB kimetenganishwa kutoka kwa HiLight, unaweza kukirudisha kwa urahisi kupitia nafasi wazi iliyo nyuma.

AINISHO LA KIUFUNDI

Seli za nishati ya jua	Silikoni ya Fuwele Moja ya 2.4 W
Fursa ya kutoa	USB ya kawaida (5 V, 1 A)
Ingizo	Mwangaza wa Jua au kupitia USB Ndogo (5 V, 1 A)
Betri	14 Wh Li-Po (3900 mAh, 3,7 V)
LED	1 W LED Bora
Hali joto ya utendaji	Sentigredi -5 mpaka + 60°
Kadiri	Kipenyo sentimita 19 kina sentimita 2.5
Uzito	Gramu 430
Uthibitisho	Iliyothibitishwa na CE, tiifu kwa RoHS

USULUHISHAJI

Tatizo	Suluhisho
HiLight haichaji kifaa chako	Betri la ndani linaweza kuwa tupu. Jaribu kuchaji betri kupitia mwangaza wa jua au lango la USB ndogo.
	Kebo ya kuchaji sio tangamani. Jaribu kutumia kebo inayofaa (USB ya Kawaida).
	Kifaa chako chaweza kutumia nguvu zaidi kuliko kile cha HiLight. Unganisha tu vifaa vinavyofaa kulingana na ainisho.
LED ya HiLight haiwaki.	Betri la ndani linaweza kuwa tupu. Chaji betri kupitia mwangaza wa jua au lango la USB ndogo.
LED nyekundu imewaka.	Kama kuna zaidi ya kifaa kimoja ambavyo vimeun-ganishwa, tenganisha vyote na unganisha kimoja peke yake.
	Wenn HiLight Batterie außerhalb der Betriebstem-peratur liegt (-5 to + 60°C), stellen sie HiLight an eine kältere/wärmere Stelle bis rotes LED erlischt.

MAAGIZO YA USALAMA
- HiLight huelea, lakini haifai kuingizwa au kutumiwa chini ya maji. Kama maji yameingia ndani ya bidhaa, wacha ikauke kabisa kifuniko cha USB kikiwa kimefunguliwa kabla ya kutumiwa. Kama sivyo mfumo wa kielekt-roniki umaweza kuhariibika.
- Utumizi wa nishati wa kifaa unachochaji unafaa uwe wa upeo wa juu wa 5 V DC, 1 A.
- Ukichaji HiLight kutoka kwa gridi au USB hakikisha unatumia kebo iliyohalalishwa na iliyojaribiwa na CE, inayofaa kwa mahali pako na gridi ya umeme. Kama sivyo HiLight yako inaweza kuharibika.
- Weka vitu vya kuwaka au vya kulipuka mbali na HiLight.
- Epuka kuwekelea vitu vizito juu ya Hilight.
- Usitumie HiLight kama imeharibika.
- Chomoa HiLight kutoka kwa gridi au kebo ya USB wakati betri imejaa.
- Usitupe HiLight kwa kuichoma au pamoja na taka za nyumbani.

HATI YA KUBADILISHA BIDHAA
Hi Nation haitwai wajibu wowote wa matumizi yasiyofaa ya HiLight au kifaa chochote kingine kilichounganishwa kwa HiLight. Kuchakaa na kuisha kwa betri hakujakingwa na hati hii. Kama unaamini kwamba uko na haki ya kutengenezewa au kubadilishiwa HiLight yako, kwa msingi wa haki zako za kisheria na sheria za kitaifa zinazohusika na uuzaji wa bidhaa za wateja, tafadhali wasiliana na mwuuzaji wako.

Kwa maelezo zaidi na kupata mwuuzaji wa eneo lako, angalia www.hination.com

UTUPAJI WA BIDHAA
Bidhaa hii haifai kutupwa na taka za nyumbani. Bidhaa inafaa itupwe kwa njia sawa na ile ya vifaa vyovyote vya kielektroniki vilivyo na betri na viambajengo vya kielektroniki

TANGAZO LA KUTII
Hi Nation AB inatangaza kwamba bidhaa hii inafuata mahitaji na matoleo muhimu ya Maelekezo 2004/108/EC.